# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# BUNGE LA TANZANIA

## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

## KIKAO CHA ISHIRINI NA SABA

**19 MEI, 2025**

## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

---

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

### KIKAO CHA ISHIRINI NA SABA - TAREHE 19 MEI, 2025

**I. DUA:**

**II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 pamoja na Maoni ya Kamati

kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

## III. MASWALI:

## OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

**339 MHESHIMIWA DKT. CHARLES STEPHEN KIMEI (VUNJO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itafanya ukarabati na kuongeza majengo ya Maabara katika Kituo cha Afya cha Mwika.

**340 MHESHIMIWA MASHIMBA MASHAURI NDAKI (MASWA MAGHARIBI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Kituo cha Afya Mwasayi ambacho kimepelekewa Vifaa Tiba lakini hakina majengo ya kutosha.

**341 MHESHIMIWA REHEMA JUMA MIGILLA (ULYANKULU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itajenga Sekondari nyingine katika Kata ya Kanindo kwa kuwa Shule ya Sekondari Kanindo ina Wanafunzi wengi.

**OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):**

**342 MHESHIMIWA ALLY JUMA MAKOA (KONDOA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira):-

Je, lini Serikali itaanza kazi ya kurejesha Mto Kondoa katika njia yake ya asili.

**343 WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:**

**MHESHIMIWA SEIF KHAMIS SAID GULAMALI (MANONGA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo:-

Je, lini Serikali itatoa fedha za ujenzi wa Viwanja vya Michezo Sekondari ya Ziba – Manonga.

## WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA:

**344 MHESHIMIWA OLIVER DANIEL SEMUGURUKA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kufufua Kiwanda cha *Ngara Arab Globe* cha kuchakata Kahawa ghafi ili kuongeza thamani ya Zao la Kahawa.

## WIZARA YA UCHUKUZI:

**345 MHESHIMIWA MAULID SALEH ALI (WELEZO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi:-

Je, lini Serikali itajenga uzio wa umeme kwenye Reli ya SGR kutoka Ngerengere hadi Dodoma.

## WIZARA YA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:

**346 MHESHIMIWA TAMIMA HAJI ABASS (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari:-

Je, upi mpango wa Serikali kuimarisha mawasiliano ya simu kwenye Vijiji vyenye changamoto ya huduma hiyo Mkoa wa Kaskazini Unguja.

**WIZARA YA UJENZI:**

**347 MHESHIMIWA SHANIF JAMAL MANSOOR (KWIMBA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Serikali itatoa fedha za ujenzi wa Barabara ya Magu – Ngudu - Hungumarwa Km 10 ambapo Mkataba ulishasainiwa.

**348 MHESHIMIWA JOSEPHINE JOHNSON GENZABUKE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Serikali itajenga Daraja la Mto Malagarasi katika Tarafa ya Ilagala - Uvinza.

**349 MHESHIMIWA GODWIN EMMANUEL KUNAMBI (MLIMBA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Mkandarasi atapatikana na kuanza ujenzi wa Barabara ya Morogoro hadi Njombe *Border* kutoka Ifakara hadi Chita.

**WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:**

**350 MHESHIMIWA BONNAH LADISLAUS KAMOLI (SEGEREA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum:-

Je, namna gani Serikali inatekeleza takwa la Sera la ushirikishwaji wa Wazee katika shughuli za uzalishaji mali.

## IV. HOJA ZA SERIKALI:

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:**

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

| | |
|---|---|
| **DODOMA** | **BARAKA I. LEONARD** |
| **19 MEI, 2025** | **KATIBU WA BUNGE** |

PARLIAMENT OF TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA